

JINA: .....DARASA:.....NAMBARI:.....

**KIDATO CHA KWANZA.**

**1. UFAHAMU (ALAMA 10)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

**KAWI**

Kuenezwa kwa huduma za nguvu za umeme ni kigezo muhimu cha kupimia kiwango cha maendeleo katika maeneo mengi nchini. Hali hii imetokana na wingi wa shughuli zinazoambatisha aina hii ya kawi. Shughuli hizi ni pamoja na zile za kibinafsi nyumbani, viwandani na kwenye asasi mbalimbali. Aidha, nguvu za umeme zinazidi kuhitajika kila uchao hasa katika sekta ya Tehama. Kukosekana kwa huduma hii muhimu hata kwa muda mfupi huwa na athari kubwa.

Njia kuu ya uzalishaji wa nguvu za umeme ni ile ya kutumia mitambo inayoendeshwa kwa maji. Katika miaka ya hivi majuzi uzalishaji wa aina hii umekumbwa na uhaba wa maji kwenye mabwawa. Baadhi ya vituo vya kuzalishia umeme vimelazimika kufungwa. Ukosefu wa mvua ya kutosha umetokana na mabadiliko ya hali ya anga. Kukosekana kwa uhifadhi wa misitu na vyanzo vya chemichemi na mito ndiko kulikochangia pakubwa katika kupungua kwa maji kwenye mito na hatimaye kwenye mabwawa.

Kutokana na hali ilivyo sasa, ni dhahiri kuwa lazima vyanzo vya kawi mbadala vitafutwe. Kawi mbadala itahitajika ili kudumisha na kuimarisha kiwango cha maendeleo kitakikanacho.

Kawi mbadala inayopendekezwa itafitiwe ni ile itokanayo na jua. Sehemu nyingi za nchi huwa na mihula mirefu ya jua. Jua ni chanzo muhimu cha kawi. Vioo na betri maalumu huweza kuvuna kawi hii isiyoiisha kutoka kwa jua. Inaweza kutoa huduma za nguvu za umeme kwa matumizi mbalimbali. Sehemu ambazo zimependekezewa aina hii ya kawi ni zile zilizo mbali na mtandao wa nguvu za umeme za kawaida. Manufaa makubwa ya kawi ya jua ni kuwa mtumizi hahitaji kulipa bili yoyote. Hata hivyo, uwekezaji wa awali unaweza kuwa na gharama kubwa hasa kwa mtu binafsi.

Kawi mbadala nyingine ni ile inayotokana na mvuke. Uzalishaji wa kawi hii umeegemezwa kwenye matumizi ya mitambo inayoendeshwa kwa mvuke. Nchini kuna vyanzo vingi vya mvuke hasa katika eneo la bonde la ufa. Nguvu za umeme zizalishwazo huunganishwa kwenye mtandao wa kitaifa. Kampuni inayotegemewa kuzalisha na kuimarisha kawi nchini humu ni Kengen.

Chanzo kingine cha kawi mbadala ni upepo. Matumizi ya upepo yamekuweko kwa karne nyingi katika mataifa ya Bara Uropa. Ajabu ni kwamba humu nchini hayajastawishwa ipasavyo. Nchi hii ina maeneo mengi ambayo yameinuka na tambarare ambako upepo huvuma kwa nguvu nyakati nyingi za mwaka. Tangu zamani upepo umekuwa ukitumiwa kuzungushia mapanka makubwa yaliyoendesha mitambo mbalimbali. Baadhi ya mitambo hiyo ni vinu vya kusagia nafaka. Mitambo ya kupasua mbao au kutoa maji visimani. Utafiti uliofanywa umeonyesha kuwa mapanka haya haya yaendeshwayo kwa upepo yanaweza kuendesha mitambo ya kuzalisha nguvu za umeme.

Njia zingine zitakazovumbuliwa zikiimarishwa nchi yetu itaacha kuwa tegemezi kwa mvua isiyotabirika. Hali hii itachangia katika uimarishaji na udumishaji wa kasi ya maendeleo.

**Maswali**

- a) Taja sehemu tatu ambako kawi ya umeme hutumiwa. (ala 3)

- b) Eleza changamoto inayoikumba nchi inayotegemea maji kama chanzo cha kawi. (ala 1)
- c) Mbali na maji, taja vyanzo vingine vya kawi. (ala 3)
- d) Kwa mujibu wa taarifa, andika matumizi matatu ya kawi ya upepo. (ala 3)

**SARUFI (ALAMA 15)**

1. Tofautisha kati ya irabu na konsonanti. (ala 2)
2. Taja sifa bainifu za irabu zifuatazo. (ala 2)
- a) /o/
- b) /e/
3. Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti sighuna. (ala 2)
4. Taja vipashio vya lugha. (ala 2)
5. Andika kwa wingi (ala 1)  
Mtoto mvulana angali anacheza kandanda.

6. Andika neno lenye mpangilio ufuatao wa silabi.  
(a) KKKI  
  
(b) KKI (ala 2)
7. Bainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (ala 2)  
Mwanafunzi mrefu anavuka barabara.
8. Tofautisha kati ya ala tuli na ala songezi na utolee mifano. (ala 2)

**ISIMU JAMII (ALAMA 5)**

- i. Ni nini maana ya Isimu Jamii. (ala 1)
- ii. Eleza maana ya sajili / Regista. (ala 1)
- iii. Taja kaida zozote tatu za lugha. (ala 3)